# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
# CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**021**

## KISWAHILI
(Kwa Watahiniwa walioko Shuleni tu)

*MUDA: Saa 3* *Alhamisi, 8 Oktoba 2009 asubuhi*

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni la lazima.
3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi.

## SEHEMU A (Alama 10)

## UFAHAMU

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.

Kwa neno zima uzalendo ni mapenzi ya nchi. Mapenzi haya hayafanyiki kwa njia za kubuniwa na watu lakini yamekwishatangulia kuwa katika mioyo yetu. Uzalendo ni tabia ya maumbile, nasi tunayo toka wakati wa kuzaliwa. Tunafikiri habari za nchi yetu kama tufikiriavyo habari za baba na mama zetu; kwa hivi kila mtu anajali sana mahali alipozaliwa.

Baadhi ya watu hawakubali nao wako tayari siku zote kupinga pishi ya hoja zako kwa ukufi wa hoja zao. Wao hufikiri kwamba uzalendo ni maono ya ushupavu na dalili ya uchache wa ustaarabu wa moyo. Kwao uzalendo ni imani ya kishenzi, kwa sababu hutenga kando nchi nyingine.

Wanadai kwamba mtu ni lazima apende ulimwengu mzima na watu wa ulimwengu hufanya kila mtu kuwa raia wa dunia si wa mahali pake padogo pajulikanapo kama nchi yake. Lazima niseme kweli kwamba wazo la udugu wa ulimwengu ni bora kwa makisio lakini kwa matumizi haliwezekani. Bora katika watu ni yule apendaye nchi yake kwanza. Kuna mashaka makubwa kama mtu anaweza kuamini katika mapenzi ya udugu wa ulimwengu bila kupenda nchi yake ikiwa hivyo, uzalendo huthibitisha ubora wa kupenda sehemu ya ulimwengu ambayo ndani yake tumezaliwa.

Mapenzi ya mtu kwa nchi yake hayaoneshi chuki ya nchi nyingine za ulimwengu. Uzalendo wa uwongo ndiyo utufanyao kuchukia nchi nyingine. Aidha, lazima tupende nchi zetu kwa sababu ya nchi zenyewe. Pasiwe na kusudi baya au la choyo nyuma yake. Kuna uzalendo wa uwongo vilevile ambao ni hila tufanyayo kwa makusudi yetu wenyewe ya choyo kwa sababu ya nia mbaya za kujitajirisha. Uzalendo wa kweli hutokana na mapenzi yasiyo na choyo ya nchi zetu na heshima yetu ya historia na malezi. Uzalendo usitufanye kujiona kwamba sisi ni watu azizi ulimwenguni na makabila mengine yote si kitu.

Mapenzi ya nchi zetu huonekana kama maono bora lakini hayana maana kama hayachukuani na matendo. Uzalendo wa matendo tu ndio wenye thamani nchini iwapo katika hatari ya shambulio la adui. Mapenzi ya mtu kwa nchi yasiyo ya matendo yanaweza kuwa mema katika nyakati za amani, lakini katika nyakati za vita uzalendo huthibitisha unyofu wake katika kitali. Uzalendo hutaka sadaka za maisha, jamaa, mali na kila kitu cha mtu. Watu wanaotoa sadaka za maisha yao kwa sababu ya nchi zao ni mashahidi.



tata print uk.

**Maswali**

(a) Mwandishi ana msimamo gani kuhusu uzalendo?
(b) Mwandishi anatoa angalizo gani kuhusu uzalendo?
(c) "Kupinga pishi ya hoja zako kwa ukufu wa hoja zao." Usemi huu una maana gani kulingana na habari uliyoisoma?
(d) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa kifungu cha habari ulichosoma.

2. Andika muhtasari wa aya mbili (2) za mwisho za habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi sitini (60).

## SEHEMU B (Alama 25)

## SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Vitenzi vya Kiswahili vina tabia zake. Kwa kutumia mifano ya sentensi tano (5) onesha tabia tano (5) tofauti za vitenzi.

4. Kuna tofauti gani kati ya mofimu huru na mofimu tegemezi? Eleza kwa kutumia sentensi nne (4), mbili (2) kwa kila mofimu.

5. (a) Eleza maana ya vidahizo vifuatavyo:
   (i) Kinyenyezi
   (ii) Matandu
   (iii) Matlaba
   (iv) Sandali
   (v) Uzimbezimbe.

   (b) Tunga sentensi moja (1) kwa kila kidahizo.

6. Vitenzi vishirikishi hukamilisha ujumbe katika sentensi. Kwa kutumia mifano mitano (5) thibitisha ukweli huo.

7. Fafanua dhana ya kiunganishi huru. Kwa kutumia mifano dhihirisha tofauti kati ya kiunganishi huru na aina nyingine ya kiunganishi.

print uk.

## SEHEMU C (Alama 10)

## UANDISHI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Andika insha yenye maneno 250 kuhusu moja ya mada zifuatazo:
   (a) Aisifuye mvua imemnyeshea.
   (b) Elimu ya msingi ina umuhimu wake katika jamii.
   (c) Maradhi yanavyorudisha nyuma maendeleo ya familia hatimaye Taifa.
   (d) Kuelimika kwa msichana ni kuelimika kwa jamii.
   (e) Wanyama pori.

9. Katika kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwako, unahitaji marafiki kwa ajili ya kusherehekea siku hiyo. Andaa kadi ya mwaliko ili kuwapa taarifa rafiki zako.

## SEHEMU D (Alama 10)

## MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu swali la **kumi (10).**

10. Baada ya Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya taifa vyombo mbalimbali viliundwa kwa lengo la kukuza na kueneza Kiswahili. Fafanua kuhusu uundwaji wa asasi tano (5) zilizoanzishwa kwa minajili hiyo.

## SEHEMU E (Alama 45)

## FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

11. Andika methali tatu (3) zinazofanana na methali isemayo "Kata pua uunge wajihi" kisha ueleze maana na umuhimu wa methali hii katika jamii.

12. Linganisha na linganua miundo iliyotumiwa na waandishi wa diwani mbili (2) ulizosoma kati ya hizo zilizoorodheshwa.



tata print uk

13. Lugha anayoitumia mwandishi katika kazi yake ya fasihi ndiyo inayosaidia katika kufikisha wazo lake kwa hadhira. Kwa kutumia riwaya teule mbili (2) ulizosoma, jadili jinsi wasanii wa riwaya hizo walivyotumia kipengee cha tamathali za semi.

14. Jadili kufaulu na kutofaulu kimaudhui kwa waandishi wawili (2) wa tamthiliya teule ulizosoma.

15. Umeteuliwa kushiriki katika shindano la uandishi wa ngonjera la Afrika ya Mashariki. Tunga ngonjera yenye beti nne (4) kuhusu maandalizi ya uchaguzi wa mwaka 2010.

## ORODHA YA VITABU

**Ushairi**

| | |
|---|---|
| Wasakatonge | - M.S. Khatibu (DUP) |
| Malenga Wapya | - TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya Chekacheka | - T.A. Mvungi (EP & DLTD) |

**Riwaya**

| | |
|---|---|
| Takadini | - Ben Hanson (MBS) |
| Watoto wa Mama N'tilie | - E. Mbogo (H.P) |
| Joka la Mdimu | - A.J. Safari (H.P) |

**Tamthiliya**

| | |
|---|---|
| Orodha | - Steve Raynolds (MA) |
| Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe | - E. Semzaba (ESC) |
| Kilio Chetu | - Medical Aid Foundation (TPH) |

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**021**

# KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni tu)

**Muda: Saa 3** **Jumanne, 05 Novemba 2013 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni la lazima.
3. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A (Alama 10)

## UFAHAMU

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Baba alikuwa na wajibu maalum wa kuhakikisha usalama wa familia yake. Ilimbidi awe na nyumba watakamoishi mke na watoto. Nyumba zilijengwa kwa mitindo tofauti katika sehemu mbalimbali hapa nchini. Wanyakyusa walikuwa na ujenzi wao ambao ni tofauti na ule wa Wahaya. Wote wakijenga kwa ufundi wa kuvutia sana. Serikali yetu imehifadhi kwa njia ya makumbusho nyumba zilizojengwa na wakazi wa sehemu mbalimbali hapa nchini wakitumia mitindo yao ya asili. Nyumba hizi zipo katika kijiji cha makumbusho kilichopo nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Baba akishirikiana na mama walikuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa jamii yao ilipata chakula cha kutosha. Mapema watoto nao walishiriki katika shughuli za kutafuta na kuandaa chakula.

Jamii nyingine hapa nchini zilikuwa zikishughulika na ufugaji tu. Maisha na utajiri wa jamii hizi ulitegemea wanyama. Tangu utoto wao, mafunzo makuu yalihusu ufugaji. Kwa mfano, mtoto wa kimasai alijifunza kuchunga na kulinda wanyama wake tangu utotoni. Ilimbidi awe askari hodari, aweze kupambana na maadui waliotaka kuteka wanyama wao. Alitakiwa aweze kupigana na wanyama wakali porini wenye kuishambulia mifugo. Kumuua simba ilikuwa ni ishara kubwa ya uhodari wa kijana wa kimasai. Mafunzo ya kumwandaa kijana huyo, tangu utoto wake kwa kazi zitakazomkabili katika maisha, yalichukua sehemu kubwa ya malezi.

Kijana wa Kihaya alikabiliwa na mazingira tofauti sana na yale ya mwenzie wa kimasai. Wahaya ni wakulima, ufugaji ulichukua sehemu ndogo tu katika shughuli zao za kiuchumi. Wahaya hulima mazao ya kudumu kama vile migomba, mashamba yao yalihitaji ulinzi na utunzaji mzuri. Hivyo serikali imara yenye kuhakikisha amani katika nchi ili raia waweze kuendelea na kazi za kilimo kwa amani, ilihitajika. Pia Wahaya walihitaji nyumba za kudumu; maana hali ya maisha yao haikuruhusu uhamaji wa mara kwa mara kama vile Wamasai. Kwa hiyo mafunzo kamili yalihitajika ili kuwaandaa watoto kwa maisha ya namna hiyo.

Maisha katika sehemu mbalimbali katika nchi yalilazimu ziwepo njia maalum za kuwalea, kuwafundisha na kuwaandaa watoto kwa yale yatakayowakabili katika siku za usoni.

**Maswali**

(a) Eleza faida mbili zinazoweza kupatikana kwa kuhifadhi mitindo ya nyumba za asili katika kijiji cha makumbusho.

(b) Unafikiri ni sababu gani iliifanya jamii ya Kimasai kuhamahama?

(c) Kwa mujibu wa habari uliyoisoma vijana walikuwa na jukumu gani katika jamii zao?

(d) Andika kichwa cha habari kisichozidi maneno matano kinachofaa kwa habari uliyoisoma.

(e) Andika methali ya Kiswahili inayoendana na aya ya mwisho ya habari uliyoisoma.

2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi mia moja (100).

## SEHEMU B (Alama 25)

## SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Onesha nomino katika tungo zifuatazo kisha bainisha ni aina gani ya nomino:
   (a) Hatuna budi kumshukuru Mola.
   (b) Mazao yamestawi shambani.
   (c) Uzalendo usisitizwe shuleni.
   (d) Mpeleke mtoto ndani.
   (e) Nimechoshwa na upweke.

4. Andika tungo zifuatazo kwa usahihi:
   (a) Mwenyekiti alihairisha kikao.
   (b) Mtoto amedumbukia shimoni.
   (c) Kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia deksi.
   (d) Mama amenunua dazani ya sufuria.
   (e) Mwanafunzi msafi amepewa zawadi.

5. Tambulisha viambishi vyenye dhima zilizowekwa kwenye mabano katika maneno yafuatayo:
   (a) Hakukumbuka (njeo ya wakati uliopita)
   (b) Wamekamatana (kauli ya kutendana)
   (c) Akisema (hali ya masharti)
   (d) Ananiona (kurejesha mtendwa)
   (e) Tuliwashangilia (kurejesha watenda)
   (f) Huimba (hali ya mazoea)
   (g) Wamelima (wakati uliopita hali timilifu)
   (h) Wanatucheka (urejeshi wa watendwa)
   (i) Hawakusoma (ukanushi)
   (j) Amenipigisha (kauli ya kutendesha)

6. Onesha maana tano za neno "kata" na kwa kila maana tunga sentensi moja.

7. "Upatanisho wa kisarufi ni kigezo kimojawapo kati ya vigezo vya kuunda ngeli za nomino." Thibitisha dai hilo kwa kutunga sentensi ukitumia ngeli zifuatazo:
   (a) U-I
   (b) LI-YA
   (c) U-ZI
   (d) I-ZI
   (e) U-YA

## ORODHA YA VITABU

**Ushairi**

| | | |
|---|---|---|
| Wasakatonge | - | M.S. Khatibu (DUP) |
| Malenga wapya | - | TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya Chekacheka | - | T.A Mvungi (EP& D.LTD) |

**Riwaya**

| | | |
|---|---|---|
| Takadini | - | Ben Hanson (MBS) |
| Watoto wa mama N'tilie | - | E. Mbogo (H.P) |
| Joka la Mdimu | - | A.J. Safari (H.P) |

**Tamthiliya**

| | | |
|---|---|---|
| Orodha | - | Steven Raynolds (MA) |
| Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe | - | E. Semzaba (ESC) |
| Kilio Chetu | - | Medical Aid Foundation (TPH) |

## SEHEMU C (Alama 10)

## UANDISHI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Wewe ni mfanyabiashara mashuhuri mjini Dodoma. Andika barua ya kutuma bidhaa kwa mteja wako aitwaye Dunia Msimbo anayeishi Lindi. Jina lako liwe Nyila Sasisha.

9. Andika tangazo kwenye gazeti la Rai ukitoa taarifa kuhusu kupotea kwa mwanao aitwaye Raha Karaha, jina lako liwe Furaha Machupa.

## SEHEMU D (Alama 10)

## MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu swali la **kumi (10)**

10. Kwa kutumia hoja tano, onesha juhudi za Wajerumani katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini wakati wa utawala wao.

## SEHEMU E (Alama 45)

## FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

11. Fafanua matatizo matano ya kuhifadhi kazi za fasihi simulizi kwenye kanda za kunasa sauti.

12. "Mshairi siku zote hukemea uonevu katika jamii." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya diwani mbili ulizosoma.

13. "Fasihi ni chuo cha kufundisha maisha kwa jamii husika."Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila riwaya kati ya riwaya mbili ulizosoma.

14. Chagua wahusika watatu wa kike, kutoka katika kila tamthiliya kati ya tamthiliya mbili ulizosoma, kisha onesha kukubalika kwao kama kielelezo cha maisha katika jamii.

15. Tunga tenzi yenye beti tano kuhusu ongezeko la watoto wa mitaani.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

021

# KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa Wasiokuwa Shuleni tu)

**Muda: Saa 3:00** **Ijumaa, 20 Novemba 2015 mchana**

## Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni la lazima.
3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A (Alama 10)

## UFAHAMU

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.

Suala la kuwapenda na kuwajali watoto ni muhimu sana katika jamii. Leo hii suala la kuwaonesha watoto mapenzi limekuwa ni jambo la ziada kwa watu na familia nyingi. Kuna mambo mengine mengi maishani mwetu ambayo watu wengi huyaona kuwa muhimu zaidi badala ya watoto.

Kuna vitendo vingi vya ukatili ambavyo watoto hutendewa. Hivi majuzi kumekuwa na visa vya watoto wengi wachanga kutupwa majalalani. Viumbe hawa walipokatiziwa uhai, maiti zao zilitupwa kama takataka na hiyo ni miili ambayo ilipatikana jalalani. Lakini wengi wanajiuliza kuna maelfu mangapi ya miili mingine kama hiyo inayotupwa? Hili lilikuwa tone dogo la bahari ya dhambi ambazo sote tunaogelea ndani. Ni vema kila mtu kwa nafasi yake katika jamii, kuwaokoa watoto wetu, ili tusije tukawalilia baadaye.

Mambo kama haya ni mazao ya mimea yetu ambayo tuliipanda sisi ambao hatuchelewi kujiita watu walio huru, walio na maendeleo na wa kisasa. Tumekuwa watu wa kupuuza mambo ya kimapokeo ya kuzingatia utu na kuficha aibu. Aghalabu tumejitia usasa kwa kutazama filamu na video zisizokuwa na maadili, kusikiliza muziki wenye maneno yasiyokuwa na maadili. Tunapoona watoto wetu wakitembea nusu uchi, hatushughuliki hata kidogo kuwakanya na matokeo yake ni hapo tulipofikia sasa. Kama ni kosa, sisi sote tumehusika kwa njia moja au nyingine. Ni vizuri tuelewe kuwa sisi ni watunzaji na walezi wa ndugu zetu kwa kila njia.

Tutawaokoa watoto kwa kukataa mambo yote yanayowanyanyasa. Lazima tuwaoneshe watoto mapenzi. Mapenzi si chakula, mavazi na makazi tu. Mapenzi si kuwaachia vijana uhuru watende wapendavyo. Mapenzi sio kuwanunulia vitu vya bei ghali au kuacha kuwakemea wanapokosa mwelekeo. Mapenzi kwa watoto ni kuwaheshimu na kuwatendea kama binadamu yeyote. Lazima mzazi akumbuke kwamba mtoto hujifunza kutoka kwake. Mtoto atamtendea mzazi jinsi alivyotendwa. Aidha, jinsi mzazi anavyomtendea mtoto wake ndivyo atakavyowatendea watoto wake na wale wote ambao atapata kuhusiana nao kwa njia moja au nyingine.

Wazazi ni lazima wawaokoe watoto wao katika viwango vyote vya ukuaji, kusiwe na mwanya baina ya mzazi na mtoto. Watoto waweze kuwaambia wazazi yote yanayowahangaisha mioyoni mwao, na hali hii itawapa wazazi fursa ya kuwasaidia. Mtoto anapokosa wazazi wawe tayari kumwonesha kosa lake na kumwadhibu kwa mapenzi.

Mtoto mwingine yeyote akipotoka wazazi wawe tayari kumkosoa na kuwaarifu wazazi wake. Tuache ubinafsi wetu, tukumbuke kuwa mwana wa mwenzio ni wako pia. Ni jambo la busara kuhakikisha kwamba kama wazazi, tuzingatie haki zote za watoto.

**Maswali**

(a) Pendekeza kichwa kinachofaa kwa habari hii kisichozidi maneno manne.

(b) Fafanua chanzo cha mienendo isiyofaa kwa vijana kama kilivyoelezwa na mwandishi.

(c) Kwa nini mwandishi anasema sisi sote tumehusika na mienendo mibaya ya watoto wetu?

(d) Mwandishi anatoa msimamo gani kwa wazazi kuhusu suala la mapenzi katika malezi ya watoto wetu.

(e) "Mtoto wa mwenzetu akipotoka, pia tuwe tayari kumkosoa." Unafikiri kwa mazingira ya sasa inawezekana? Toa maoni yako.

2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno mia moja (100).

## SEHEMU B (Alama 25)

## SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Sentensi zifuatazo zina makosa. Onesha kosa kisha andika upya sentensi hizo kwa usahihi.

(a) Nimekwenda kwa Kondo na nimemkuta hayupo.

(b) Dhumuni la Ali ni kuishi mjini.

(c) Tunachukua nafasi hii kuwakaribisha hapa nyumbani.

(d) Mahusiano mazuri hujenga undugu.

(e) Ni muhimu tukaelewa taratibu za lugha yetu.

4. Kuna njia nyingi za kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili. Eleza njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo:

(a) Msikwao

(b) Jografia

(c) Chemshabongo

(d) Mchezaji

(e) Kisimbuzi.

5. Tumia maneno yaliyowekwa kwenye parandesi kuunganisha sentensi zifuatazo: (**kwa**; **licha ya**; **pasi na**; **pamoja na**; **kwa sababu**)

(a) Kijana huyu anaingia chumbani. Kijana anaingia bila hodi.

(b) Juma hakusalimia wazee. Juma hakuwaona wazee.

(c) Rashidi ni mrefu. Mimi ninamshinda kwa mbio.

(d) Wewe ni mwanafunzi lakini lazima ulipe nauli.

(e) Mchezaji amerusha mpira. Mchezaji amefuata utaratibu.

6. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya utumizi wa lugha.

(b) Taja mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuteua lugha ya kutumia, kisha toa mifano miwili kwa kila moja.

7. Fafanua maana ya neno "**bichi**" kama lilivyotumika katika tungo zifuatazo kwa kuzingatia muktadha husika:

(a) Niletee shuka la kijani **kibichi.**

(b) Hili embe bado ni **bichi**.

(c) Msichana huyu ni **mbichi** kabisa.

(d) Chakula hiki ni **kibichi**.

(e) Koti lake ni **bichi**.

## SEHEMU C (Alama 10)

## UANDISHI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Andika insha isiyopungua maneno mia mbili hamsini (250) na isiyozidi maneno mia tatu (300) kuhusu "Madhara ya Operesheni Kimbunga."

9. Andika mambo ya kuzingatia katika kuandika kumbukumbu za mkutano wa mara ya pili.

## SEHEMU D (Alama 10)

## MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu swali la **kumi (10)**.

10. Kwa kutumia hoja nne, eleza jinsi misafara ya biashara ilivyofanikisha kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania kabla ya uhuru.

## SEHEMU E (Alama 45)

## FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**

| | | |
|---|---|---|
| **Wasakatonge** | - | M.S. Khatibu (DUP) |
| **Malenga Wapya** | - | TAKILUKI (DUP) |
| **Mashairi ya Chekacheka** | - | T.A. Mvungi (EP & D.LTD) |

**RIWAYA**

| | | |
|---|---|---|
| **Takadini** | - | Ben J. Hanson (MBS) |
| **Watoto wa Mama N'tilie** | - | E. Mbogo (H.P) |
| **Joka la Mdimu** | - | A.J.Safari (H.P.) |

**TAMTHILIYA**

| | | |
|---|---|---|
| **Orodha** | - | Steve Reynolds (MA) |
| **Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe** | - | E. Semzaba (ESC) |
| **Kilio Chetu** | - | Medical Aid Foundation (TPH) |

11. Tanzu za Fasihi simulizi huhusisha pia michezo ya watoto. Eleza faida tatu na hasara tatu za michezo ya watoto katika jamii.

12. "Mfumo wa unyonyaji katika jamii hupingwa na washairi." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya diwani mbili ulizosoma.

13. "Uongozi mbaya husababisha maendeleo ya jamii kurudi nyuma." Thibitisha kauli hiyo kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila kitabu kati ya vitabu viwili vya riwaya vilivyoorodheshwa.

14. "Waandishi wa tamthiliya wamefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kipengele cha muundo." Fafanua kauli hii kwa kutumia vipengele vitatu vya muundo kwa kila kitabu kutoka katika tamthiliya mbili miongoni mwa zilizoorodheshwa.

15. Andika ngonjera isiyozidi beti sita kuhusu "Wakazi waishio Mabondeni".

*Namba ya mtahiniwa* ……………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**MTIHANI WA ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA PILI**

**021**

# KISWAHILI

**Muda: Saa 2:30** **Jumatatu, 16 Novemba 2015 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Majibu **yote** yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa.
4. Majibu **yote** yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.
5. Vifaa **vyote** vya mawasiliano **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| **JUMLA** | | |

*Namba ya mtahiniwa* ………………………

## SEHEMU A (Alama15)
## UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Wakati wa ukoloni mabepari wa Kijerumani walianzisha kilimo cha pamba huko Kusini mwa Tanzania. Waliwalazimisha Wamatumbi kufanya kazi katika mashamba yao. Pamba iliyopatikana ilipelekwa Ujerumani. Kama anavyosema kibarua mmoja aliyeteswa na mabepari hao, "Wakati wa kilimo kulikuwa na dhiki sana. Sisi vibarua tuliokamatwa tulikaa mstari wa mbele, tukilima. Nyuma yetu kulikuwa na **mnyapara**, kazi yake kutupiga kwa **mijeledi**. Nyuma ya mnyapara alikuwepo jumbe, na kila jumbe alisimama nyuma ya watu hamsini. Na nyuma ya majumbe alisimama Bwana Kinoo mwenyewe. Lo! Hapo shuhudia kifo."

Mjerumani alipofika nchini akaamrisha Wamatumbi kulipa kodi. Watu walimjibu, "Hudai kitu. Hatuna deni kwako. Ikiwa wewe mgeni unataka kukaa nchi hii basi ni lazima wewe utuombe sisi. Na sisi tutakuambia utoe **sadaka** kwa Miungu wetu.Wewe utatoa chochote na sisi tutaifanyia karamu Miungu kwa niaba yako; tutakupa ardhi na wewe utakuwa na mahali pa kukaa. Lakini siyo sisi wenyeji tukupe wewe sadaka. Hilo haliwezekani hata kidogo."

Juu ya dhiki zote walizopata yaani dhiki ya njaa, dhiki ya maonevu, dhiki ya kulimishwa na kupigwa, watu **walistahimili** wakavumilia kwa sababu hawakuweza kupigana, kwani hawakuwa na umoja. Vilevile walijua kuwa nguvu ya Mjerumani ilikuwa kubwa. Wakangoja.

Katika mwaka wa 1904 akaja **mtume**, jina lake Kinjeketile. Karibu na kwao Ngarambe kulikuwa na bwawa la maji katika kijito cha Mto Rufiji. Kinjeketile alipandwa na pepo aitwaye Hongo, aliyekuwa akikaa katika bwawa hilo.

Kinjeketile aliwafundisha Waafrika maana ya umoja, akawapa moyo kwa nguvu ya maji. Waafrika wakawa na umoja na nguvu. Watu wengi waliosikia jina lake walikuja kumuunga mkono.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano.
………………………………………………………………………………

(b) Eleza wazo kuu linalojitokeza katika habari uliyoisoma.
………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………

(c) Ni mambo gani yanayothibitisha kwamba ni kweli Wamatumbi waliteswa? Taja mambo matatu.

(i) ………………………………………………………………………
(ii) ………………………………………………………………………
………………………………………………………………………
(iii) ………………………………………………………………………
………………………………………………………………………

*Namba ya mtahiniwa* ……………………

(d) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma.

(i) Mnyapara……………………………………………………
(ii) Mijeledi……………………………………………………
(iii) Walistahimili……………………………………………
(iv) Sadaka……………………………………………………
(v) Mtume……………………………………………………
……………………………………………………

(e) Ni mambo gani mawili unayojifunza kutokana na habari hii?

(i) ……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………

(ii) ……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………

(f) Fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu kwa maneno yasiyozidi 40.
……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………
……………………………………………………

## SEHEMU B (Alama 15)
## UTUMIZI WA LUGHA NA USAHIHI WA MAANDISHI

2. (a) Kwa kauli zifuatazo andika **KWELI** kwa kauli iliyo sahihi au **SIO KWELI** kwa kauli isiyo sahihi.

(i) Kazi ya fasihi ni moja tu na ni ile ya kuelimisha jamii. ……………………

(ii) Kiunganishi ni neno ambalo huunganisha dhana mbili tu.
……………………

(iii) Elekeza, shikilia, shikamana, maelekezo, mshikamano, tolewa, nitakutolea, ondokeni ni maneno yaliyoundwa kutokana na mnyumbuliko. ………………

(iv) Methali ni usemi wenye pande mbili. ………………

(v) Kitendawili ni aina ya fumbo lisilotumia lugha ya picha lakini hudai jibu………………

(b) Andika tungo zifuatazo kwa usahihi:

(i) Mwalimu mkuu amewakilisha mada katika mkutano.
……………………………………………………

(ii) Nilikwenda mjini nikamkutana Maria.

……………………………………………………………

(iii) Habarini zenu mabibi na mabwana.

……………………………………………………………

(iv) Kila siku nafanyaga kazi.

……………………………………………………………

(v) Kwa kuwa sina gari nitakwenda na miguu.

……………………………………………………………

(c) Andika mifano ya kauli zinazoonesha muktadha wa rejesta zifuatazo;

(i) Hotelini……………………………………………………

……………………………………………………………

(ii) Mahakamani………………………………………………

……………………………………………………………

(iii) Dukani……………………………………………………

……………………………………………………………

(iv) Darasani…………………………………………………

……………………………………………………………

(v) Hospitalini………………………………………………

……………………………………………………………

……………………………………………………………

## SEHEMU C (Alama 15)
## SARUFI

3. (a) Nyumbua maneno yafuatayo na kuunda maneno manne kwa kila neno.

(i) Angalia ………………………… ………………………… ………………………… …………………………

(ii) Chukua ………………………… ………………………… ………………………… …………………………

(iii) Oga ………………………… ………………………… ………………………… …………………………

(iv) Kata ………………………… ………………………… ………………………… …………………………

(v) Omba ………………………… ………………………… ………………………… …………………………

(b) Tumia maneno yafuatayo kama nomino na utunge sentensi moja kwa kila neno:

(i) Starehe ……………………………………………………

(ii) Ukweli ……………………………………………………

(iii) Utaalamu …………………………………………………

(iv) Umoja ……………………………………………………

……………………………………………………………

(v) Uzembe..........................................................................

(vi) Ukarimu..........................................................................

(vii) Ushujaa ..........................................................................

(viii) Upweke ..........................................................................

(ix) Upendo ..........................................................................

(x) Furaha ..........................................................................
..........................................................................

(c) Kitenzi kikuu huweza kutumika sambamba na kitenzi kingine kukamilisha sentensi. Katika sentensi zifuatazo bainisha vitenzi vilivyotumika. Sentensi ya kwanza ni mfano:

(i) Aliyekuja atasafiri kesho.

**TS** **T**

(ii) Mgeni wangu amekwisha kuwasili.
..........................................................................

(iii) Amina hakutaka kumuudhi.
..........................................................................

(iv) Mafundi wangali wanashona viatu.
..........................................................................

(v) Wataendelea kumsubiri hadi kesho.
..........................................................................

(vi) Gari lilikuwa limeharibikia mlimani Kitonga.
..........................................................................
..........................................................................

## SEHEMU D (Alama 40)
## FASIHI SIMULIZI

4. (a) Eleza kwa kifupi maana ya dhana zifuatazo:

(i) Shairi..........................................................................
..........................................................................
..........................................................................

(ii) Vichekesho..........................................................................
..........................................................................
..........................................................................

(iii) Ngonjera..........................................................................
..........................................................................

(iv) Visasili..........................................................................
..........................................................................

(v) Mapingiti ..........................................................................
..........................................................................
..........................................................................
..........................................................................

*Namba ya mtahiniwa* ...........................

(b) Jaza nafasi iliyoachwa wazi kukamilisha methali zifuatazo:

(i) Samaki mkunje ..............................................

(ii) ..............................................................

(iii) ...........................................njaa mwana malegeza.

(iv) ...........................................hutanda na kuyeyuka.

(v) Ajidhaniaye kasimama...........................................

(vi) ........................................... usiilalie mlango wazi.

(c) Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata:

Mwanafunzi **ikibali**, mbele ya wako mwalimu.
Katika siku si mbali, utakuwa aalimu,
Kijitia **baradhuli**, baadaye ulaumu,
Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.

Usijifanye kiburi, kujifanya **chakaramu**.
Hiyo wanaita shari, ndani yake ina sumu,
Hivi hauna habari, heshima kitu adimu,
Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.

Katika hii sayari, namba moja ni elimu,
Usiipate sufuri, kisha hapo ulaumu,
Maisha haya safari, mwana ujenge timamu,
Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.

Ni walezi mashuhuri, hivyo wana umuhimu,
Wameishika nambari, kutokana na kalamu,
Usimwendeshe **chuchuri**, uidumishe nidhamu,
Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.

Mwalimu baba na mama, hilo wazi ufahamu
Hivyo tazama ndarama, zisisababishe **ghamu**,
Neno hili ni la zama, shika nakupa jukumu,
Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.

Sitapenda kukuchosha, kwa mengi kukushutumu,
Nakutakia maisha, ya shule yenye utamu,
Ili upate **bashasha**, na mema **kutakadamu**,
Mbele ya wako mwalimu, mwanafunzi ikibali.

(i) Mtunzi wa shairi hili anatoa ujumbe gani?

..............................................................................

..............................................................................

..............................................................................

(ii) Ni mambo gani matatu ambayo mwanafunzi unatakiwa kuyaepuka kama yalivyoelezwa katika shairi ulilosoma?
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................

(iii) Bainisha kituo bahari katika shairi ulilosoma.
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................

(iv) Bainisha vina vya kati na vya mwisho vya shairi ulilosoma.
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................

(v) Mshairi ana maana gani anaposema, " Neno hili ni la zama, shika nakupa jukumu."
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................

(vi) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi ulilosoma;

- Ikibali ..........................................................................................
- Baradhuli.........................................................................................
- Kutakadamu ......................................................................................
- Chuchuri...........................................................................................
- Bashasha ..........................................................................................

..........................................................................................................

## SEHEMU E (Alama 15)
## UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI

Unatarajia kwenda kumtembelea shangazi yako aitwaye Nakijwa aishiye Ikwiriri Rufiji. Andika barua kwa shangazi kumjulisha makusudio yako. Jina lako liwe Jaja Okwi, Shule ya Sekondari Ndorwe, S.L.P 1534. Kilomeni. Mwanga.

..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................
..........................................................................................................

*Namba ya mtahiniwa* ……………………………

# MKOA WA DAR ES SALAAM

## MTIHANI WA UTAMILIFU WA KIDATO CHA NNE - 2015

## KISWAHILI

**CODE: 021**

**MUDA: SAA 3:00** **JUMANNE 19 MEI, MCHANA**

### MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C ,D na E
2. Jibu maswali yote katika sehemu A,B na D, Swali moja toka sehemu C na Maswali matatu kutoka sehemu E, Swali la 15 ni lazima.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi haziruhusiwi katika chumba cha mtihani.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi.
6. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu cha kujibia.

*Karatasi hii ina kurasa 4 zenye maandishi*

## SEHEMU A: UFAHAMU (alama 10)

1. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali .

Adili alipotupwa alizama kama jiwe katika kilindi cha bahari ambacho urefu wake haukutambulika. **__Viwambo vya masikio__** yake vililia akadhani maji yalipenya sikio hata sikio, na mianzi ya pua yake yalijaa maji yaliyozuia pumzi. Macho yake yalipofumbuka vimetameta kama nyota mbinguni vilionekana katika maji. Vimetameta hivyo vilifanywa na mtikisiko wa mwili wake. Kutumbukia baharini usiku wa giza ni hatari ya kutisha sana.

Kasi ya kutupwa ilipokoma alijitazama akakata vifungo vya kamba iliyotatizwa mwilini mwake. Sasa mikono na miguu yake ilianza kufanya kazi. Nusu ya nguvu yake ilikuwa imetumika,lakini matumaini yalikuwa kamili. Adili si mkata tamaa, na kabla pumzi yake haijakwisha alikusudia **__kuebuka__**. Jaribu lilikutana na **__fanaka__**, maana kabla moyo wake haujakoma alijiona anaelekea juu ya bahari. Aliinua kichwa juu ya maji na kuhema kwa nguvu kama gari moshi. Kulipopambazuka alikuwa katika bahari iliyoghadhilika kwa dhoruba kali, na hali yake ilikuwa taabani. Kutazama hatari usoni kunavunja moyo wa mtu lakini alijikaza kiume.

Mara ile palikuja ndege aliyekuwa na umbo la kutisha akamwopoa Adili majini. Kama koleo, miguu ya ndege ilimshika kwapani akaruka naye. Fikiri wewe mwenyewe hofu aliyokuwa nayo Adili. Binafsi yake alijiona ameokoka kuliwa na papa akawa chakula cha tai. Ndege mwenyewe alipaa juu mpaka Adili akapotelewa na fahamu, fahamu yake ilipomrudia alijiona katika nyumba kubwa sana iliyokuwa nzuri ajabu.

Wasichana warembo na waliochangamka walikuwa watumishi katika nyumba hiyo. Miongoni mwao palikuwa na bibi mmoja aliyejipambanua kama malaika. Huyo alikaa juu ya kiti cha enzi kilichopambwa na **__majohari__** mbalimbali. Rangi ya mavazi yake ilikuwa fua na kichwani alivaa taji lililopigisha moyo mshindo kwa uzuri. Yule ndege alikuwapo, lakini mara ile alijigeuza msichana wa utanashati mkubwa. Msichana mwenyewe alikuwa Yule aliyezama ardhini, baada ya kuokolewa na Adili alipokuwa katika umbo la tandu na kushambuliwa na nyoka jabalini.

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

A. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari uliyosoma:-
   (i) Viwambo vya masikio
   (ii) Kuebuka
   (iii) Fanaka
   (iv) majohari

B. Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano.

C. Unafikiri ni kwaninin Adili alijitutumua akakata vifungo vya kamba iliyotatiza mwilini mwake?

D. Ni kwanini Adili alihema kwa nguvu kama gari moshi?

2. Andika muhtasari wa habari ifuatayo kwa maneno ishirini (20)

Msemakweli alihitimu masomo yake ya kidato cha nne mnamo mwaka 2011. Baada ya kuhitimu masomo yake hakupata bahati ya kuendelea na masomo ya kidato cha tano kwasababu ya ukosefu wa fedha za kumpeleka shule .Hali hiyo ilisababisha kijana huyu kuanzisha biashara ya kuuza mchicha,sukuma wiki, matembele, spinachi, majani ya kunde na uyoga. Akiwa wakati wote kwenye soko dogo la Mtakuja, Msemakweli aliendesha biashara hiyo ndogo na iliweza kumhakikishia chakula, mavazi na malazi.

## SEHEMU B: (alama 25)
## SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

3. Eleza dhima ya mofimu U iliyopigiwa mstari katika sentensi hizi.
   (a) Wewe u mtoto wa nani?
   (b) Mkate uliokula umeoza.
   (c) Sasa unamlilia nani?
   (d) Paka amemuua panya.
   (e) Kaka aliufungua mlango.

4. Unda misamiati mipya mitano (5)kwa njia ya kuambatanisha maneno.

5. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali
   - Haloo! Wale watu walikuwa wanakutafuta sana

6. Ukitumia mifano ya kueleweka andaa rejesta ya mahakamani isiyopungua Rejesta kumi (10).

7. Yapange maneno yafuatayo kama yanavyo onekana katika kamusi kisha eleza maana ya kila neno.
   (i) Makala
   (ii) Ghairi
   (iii) Mantiki
   (iv) Matabaka
   (v) Maleba

## SEHEMU C: (alama 10)
## UANDISHI

Jibu swali moja tu kutoka sehemu hii.

8. Fafanua mambo ya kuzingatia unapotaka kuandika kumbukumbu ya mkutano.

9. Tunga Insha ya kisanaa juu ya mojawapo kati ya mada hizi.
   (a) Athari za fesibuku (face book) kwa wanafunzi.
   (b) Mauaji ya Albino.

## SEHEMU D: (alama 10)

10. Jibu swali la (10) katika sehemu hii.
    Chora ramani ya upwa wa Afrika Mashariki kisha onesha maeneo ambayo lahaja hizi huzungumzwa..
    (a) Kimakunduchi
    (b) Kivumba
    (c) Kimvita
    (d) Kitikuu
    (e) Kimgao

## SEHEMU E: (alama 45)

Jibu maswali matatu tu kutoka sehemu hii. Swali la 15 ni lazima.

11. Kukua kwa sayansi na teknolojia kumesababisha fasihi simulizi kupoteza uhalisia wake. Fafanua kauli hii kwa hoja tano (5).

12. “Msanii wa fasihi huwa na lengo la kuelimisha jamii kuondokana na mabaya na kuelekea katika ujenzi wa jamii mpya yenye maendeleo na utengamano” kwa kutumia hoja tatu kutoka kila Diwani mbili ulizosoma thibitisha kauli hii.

13. Chagua wahusika wawili, mmoja toka katika kila riwaya mbili ulizosoma, kisha fafanua namna walivyochorwa kwa kuzingatia mienendo na matendo ya binadamu halisi katika maisha ya jamii ya kitanzania. Toa hoja tatu kwa kila mhusika.

14. Mwanamke ndani ya tamthiliya mbili ulizosoma amekwezwa na kutwezwa. Thibitisha kauli hii ukionesha jinsi mwanamke alivyotwezwa. Toa hoja tatu kwa kila kitabu.

15. Malizia utenzi huu mpaka zifike beti tano (5).

Kitu cha bure heshima,
Mpe baba na Mama,
Kila mtu mzima,
Na walio nawe sawa

**Orodha ya vitabu**

USHAIRI

| | |
|---|---|
| Malenga wapya | TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya chekacheka | T.A.MVUNGI(EP&D) |
| Wasakatonge | Ms. Khatibu (DUP) |

**RIWAYA**

| | |
|---|---|
| Joka la Mdimu | A.J. Safari (H.P) |
| Takadini | Ben Hanson (MBS) |
| Watoto wa Mama Ntilie | E. Mbogo (H.P) |

**TAMTHILIYA**

| | |
|---|---|
| Kilio chetu | (Medical Aid foundation) |
| Ngoswe- penzi kitovu cha uzembe | (E. Semzaba) |
| Orodha | Steve Reynolds (MA) |

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**021**

# KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Jumanne, 04 Novemba 2014 mchana**

## Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni la lazima.
3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A (Alama 10)
## UFAHAMU

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

Karibu masikio ya watu wa mahali pengi yalijaa habari za Karama na mashtaka yake. Umaarufu wake wa ghafla ulizungumzwa karibu na mbali. Mtu yeyote wa desturi anapozuka katika umaarufu, huyavuta masikio na macho ya watu wengi kwa sababu jambo kama hili hutokea nadra sana kwa watu ambao bahati mbaya imeshughulika kuwaweka nyuma. Kwa hiyo, siku ya tatu ya baraza ilihudhuriwa na mfalme, watu wenye vyeo mbalimbali, pamoja na nusu moja ya umati mkubwa wa Kusadikika. Fikra zilizochanganyika ziliushika umati huu. Baadhi ya watu walimwajabia Karama wakamhesabu kama mtu bora wa karne yao. Hawa walitumaini ataokoka lakini wengine waliwaza kuwa Karama alikuwa kama mjinga aliyekuwa akicheza na hatari kubwa iliyofunua taya mbele yake.

Waliokuwa wakimtazamia kuokoka walikuwa na wasiwasi wao; na wale waliokuwa wakimtazamia kuanguka walikuwa na **fadhaa** yao. Walakini hapana mtu hata mmoja aliyepata kulisema wazo lake.

Bila ya kujua alivyoajabiwa Karama aliendelea kusema mbele ya baraza, "Watu wanaoteswa ndio wanaoyajua mateso yao." Kusadikika ilikuwa chini ya mateso makubwa sana. Maisha yao yalizungukwa na maradhi na mauti, uadui usiokwisha, nchi iliyokaribia kugeuka jangwa na mwamba na **madhila** mengine mazito yaliyowakabili watu. Wanakusadikika walitaka faraja katika mateso haya. Kila jitihada ilijaribiwa ili kuirekebisha saa ya maendeleo ya nchi, lakini mara kwa mara majira yake yalirudishwa nyuma. Kama hili lilifanywa kwa makosa ama kwa makusudi ni siri iliyo ng'ambo ya fahamu zangu hata sasa. Lakini kama siri njema hufichika, ile iliyo mbaya haifichiki hata kidogo. Uchaguzi wa wajumbe ulikuwako lakini mathibitisho ya matokeo ya ujumbe hayakupatikana.

Kusadikika iliishi kuona mjumbe baada ya mjumbe **kuadhiriwa** na kuadhibiwa vibaya. Kama washauri hawakudhuriwa na hili lakini watu wengine walidhuriwa sana. Kazi njema za wajumbe wawili zilipotea bure. Manung'uniko ya lawama hii yalikuwa katika hewa yote ya Kusadikika.

Hili lilipotokea serikali iliombwa **ima faima** kufanya ujumbe mwingine. Basi mjumbe wa tatu alitakikana ajitolee mwenyewe kwa ujumbe wa Kusini. Wito wa mjumbe wa tatu uliitikiwa na Kabuli; mtu mwenye busara, haya na mcheshi. Yeye alipatikana upesi kabisa kuliko ilivyokuwa kwa mara ya pili na ya kwanza. Misiba ya Buruhani na Fadhili ilikuwa mikubwa ya kutosha kuikongoa mioyo ya bidii katika bawaba zake. Kabuli aliyajua haya yote lakini alikuwa mtu wa moyo wa namna nyingine kabisa. Alikuwa na bidii kubwa kama ile ya siafu athubutiye kukivuka kijito kwa daraja iliyofanywa kwa maiti ya siafu wengine walioelea majini huko na huko. Maji yalijulikana kuwa ni asili ya rutuba, mvuke na umeme. Nguvu nyingine za namna mbalimbali zipo pia katika maji. Kama siafu mdudu mdogo na kipofu wakati mwingine haogopi kuzikabili nguvu hizo pamoja na hatari zake kwa sababu njema, basi ni dhahiri kuwa viongozi wa wanadamu wanapoteswa bure bidii za wafuasi wao hutanuka ajabu.

Hapana tishio liwezalo kuukomesha mwendo huu. Kwa hakika utafululiza kuwako duniani mpaka mateso yakome kabisa, na labda wakati huo dunia hii itakuwa njema kama itamaniwavyo kuwa. Buruhani na Fadhili walitoa sadaka zao bora ili kuyahimiza majilio ya wakati uliotakikana sana. Kabuli aliwaona watu wawili hawa kama wafadhili wakubwa wa ulimwengu. Alitaka kuwa mshirika wao kwa thamani yoyote ya maisha yake.

Kama ijulikanavyo, Kusini ni upande wa dunia yatokako matufani makubwa na baridi kali sana. Kabuli aliyakabili mashaka haya bila ya **kigeugeu**. Naam, alikuwa kama mtu aliyekuwa akinywa uchungu bila ya **kigegezi**. Mara mbili alikamatwa akafanywa mahabusu.

**Maswali**

(a) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari:
- (i) Fadhaa
- (ii) Madhila
- (iii) Kuadhiriwa
- (iv) Ima faima
- (v) Kigeugeu
- (vi) Kigegezi.

(b) Eleza mchanganyiko wa fikira walizonazo wana wa Kusadikika kuhusu Karama.

(c) Kwanini bidii ya mjumbe wa Kusini imelinganishwa na bidii ya siafu? Toa sababu mbili.

(d) Ujumbe wa mwandishi wa kifungu hiki unahusu nini?

2. Fupisha habari uliyosoma katika swali la kwanza kwa maneno yasiyopungua mia moja na hamsini (150) na yasiozidi mia mbili (200).

## SEHEMU B (Alama 25)
## SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA
Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Fafanua utata uliopo katika sentensi zifuatazo:
   - (a) Mama anafurahia pango.
   - (b) Mwalimu analima barabara.
   - (c) Alimpigia ngoma.
   - (d) Kijana amepata fomu.
   - (e) Baba anaunda.

4. Tumia neno "Paa" katika sentensi kuunda dhana zifuatazo :
   - (a) Nomino
   - (b) Kitenzi
   - (c) Kielezi
   - (d) Kivumishi
   - (e) Shamirisho

5. Bainisha mzizi wa asili kwa kila neno katika maneno yafuatayo:
   (a) Anawaandikisha
   (b) Mkimbizi
   (c) Mlaji
   (d) Muumbaji
   (e) Nisingelipenda
   (f) Kuburudika
   (g) Sadifu
   (h) Aliokota
   (i) Walichopoka
   (j) Kipambanuliwe

6. Vibadilishe vitenzi vifuatavyo viwe katika kauli ya kutendeka:
   (a) Badili
   (b) Kata
   (c) Komboa
   (d) Zuia
   (e) Fika
   (f) Zoa
   (g) Jenga
   (h) Remba
   (i) Tumia
   (j) Lima

7. Fafanua maana ya neno "chenga" kwa kutumia sentensi tano tofauti.

## SEHEMU C (Alama 10)
## UANDISHI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Andika insha yenye maneno yasiyopungua mia mbili (200) na yasiozidi mia tatu (300) kuhusu methali isemayo "Samaki Mkunje angali mbichi".

9. Wewe ni mwenyekiti wa mtaa ambao umekumbwa na mafuriko lakini wananchi wako wanakataa kuhamia makazi mapya. Andaa hotuba utakayoitoa kwa wananchi wa mtaa wako ili kuwashawishi kuondoka katika sehemu hiyo. Jina la mtaa ni Kwamachombo na eneo la makazi mapya linaitwa Kitivo.

## SEHEMU D (Alama 10)
## MAENDELEO YA KISWAHILI
Jibu swali la **kumi (10)**

10. Kwa kutumia hoja tano, fafanua jinsi utawala wa Waingereza ulivyoimarisha Kiswahili nchini Tanzania kwa kupitia mfumo wa elimu.

## SEHEMU E (Alama 45)
## FASIHI KWA UJUMLA
Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

11. Kutokana na mabadiliko yanayoikumba jamii, baadhi ya methali zimepitwa na wakati. Thibitisha hoja hiyo kwa kutumia methali sita.

12. "Ustadi wa msanii hudhihirishwa na fani". Dhihirisha kauli hiyo kwa kutumia vipengele vitatu vya lugha kwa kila diwani kutoka katika diwani mbili ulizosoma.

13. Jadili kukubalika kwa wahusika wawili kama kielelezo halisi cha wanajamii kati ya Takadini, Maman'tilie na Brown Kwacha kutoka katika riwaya mbili ulizosoma. Toa hoja tatu kwa kila mhusika.

14. "Kujenga jamii bora ni dhima ya mwandishi." Thibitisha kauli hii kwa kutumia hoja tatu toka katika kila tamthiliya kati ya tamthiliya mbili ulizosoma.

15. Tunga tamthiliya fupi kuhusu umuhimu wa elimu kwa vijana wa Tanzania ya leo. Tamthiliya hiyo isipungue maneno mia tatu (300).

**ORODHA YA VITABU**

**Ushairi**

| | | |
|---|---|---|
| Wasakatonge | - | M.S. Khatibu (DUP) |
| Malenga Wapya | - | TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya Chekacheka | - | T.A. Mvungi (EP & D.LTD) |

**Riwaya**

| | | |
|---|---|---|
| Takadini | - | Ben J. Hanson (MBS) |
| Watoto wa Maman'tilie | - | E. Mbogo (H.P) |
| Joka la Mdimu | - | A.J.Safari (H.P.) |

**Tamthiliya**

| | | |
|---|---|---|
| Orodha | - | Steve Reynolds (MA) |
| Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe | - | E. Semzaba (ESC) |
| Kilio Chetu | - | Medical Aid Foundation (TPH) |